SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.24 NO. 2 2025
DOI: 10.51984/JOHS.V24I2.3825

مجلة جامعة سبها للعلوم الإنسانية
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: http://www.sebhau.edu.ly/journal/johs

# KUCHUNGUZA DHAMIRA YA MAPENZI NA KIJANA KATIKA NYINBO ZA BONGO FLEVA ZA MSANII NASIBU ABDUL

Abdulfattah Faraj Omar & Mohamed Omary Maguo

Department of Linguistics and Literary Studies, the Faculty of Arts and Social Sciences, The Open University Dar es Salaam, Tanzania.

**Maneno muhimu:**
Mapenzi
Kijana
Nyimbo
Dhamira

**Ikisiri:**

Makala haya yanahusu kuchunguza dhamira ya mapenzi na kijana katika nyimbo za bongo fleva za msanii Nasib Abdul ambaye ni msanii maarufu wa nyimbo za bongo fleva wa nchi ya Tanzania. Data za makala haya zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo na nadharia ya Saikolojia Changanuzi. Makala yamebaini kwamba kijana wa Kitanzania anasawiriwa katika kuteseka kimapenzi, mapenzi ya uongo, kubadili wapenzi na nguvu ya mapenzi. Kupitia mapenzi vijana wapo waliofanikiwa katika maisha na wapo ambao wamepata madhara kama kufariki kwa sababu tu ya mapenzi. Hii inaonesha kwamba mapenzi ni kitu chenye nguvu sana katika jamii na hasa kwa vijana.

# استكشاف موضوع الحب والشباب في أغاني بونغو فلافا للفنان نسيبو عبدول.

عبد الفتاح فرج عمر ومحمد عمري ماقو

قسم اللغويات والدراسات الأدبية، كلية الآداب والعلوم الاجتماعية، الجامعة المفتوحة دار السلام، تنزانيا.

**الكلمات المفتاحية:**
الحب
الشباب
اغانى
طرب
نية

**الملخص**

أغاني بونغو فليفا كما تُعرف تحظى بشعبية كبيرة بين الشباب الذين تتراوح أعمارهم بين الخامس عشر عامًا وما فوق (عمري، 2009). يتم تقديم الأغاني من خلال الصوت والفيديو، وتتضمن الشعر والموسيقى والغناء. بدأت هذه الأغاني، المعروفة أيضًا باسم موسيقى الجيل الجديد، في عام 1990 كمنتج لموسيقى الهيب هوب الأمريكية، الهيب هوب وهو نوع من موسيقى الراب التي غناها الأمريكيون من أصل أفريقي كوسيلة للتعبير عن آرائهم حول الكيفية التي يريدون أن يكون عليها المجتمع الأمريكي. كان المجتمع الأمريكي يعيش في مجتمع عنصري حيث تم حرمان الأمريكيين السود من الفرص المتساوية في التعليم والتوظيف والمناصب القيادية والرعاية الصحية والسكن اللائق. ومن خلال هذه الأغاني، تمكنوا من التعبير عن مشاعرهم تجاه هذا التمييز والحاجة إلى إجراء تغييرات كبيرة حتى يتمتع كل أمريكي بنفس الحقوق مثل أي شخص آخر، وفيما يتعلق بأغاني بونغو فليفا في تنزانيا، فقد استخدمها الشباب كوسيلة للتعبير عن تطلعاتهم والتحديات الحياتية التي يواجهونها، بما في ذلك البطالة والفقر والفساد وسوء الإدارة والظلم والمرض، وخاصة الإيدز. تعبر أغاني بونغو فلافا عن العديد من القضايا المتعلقة بالحياة في المجتمع، ويُذكر الحب باعتباره الأبرز. وذلك لأن الحب في فترة المراهقة هو شيء يزعج الكثير من الشباب بسبب كونها فترة التغيرات الجسدية. يزعم تومسون أنه لا ينبغي إلقاء اللوم على الشباب بسبب الحديث عن الحب لأن هذا هو وقتهم للقيام بذلك وهو أعظم احتياجاتهم في الحياة في سنهم. هذه المعلومات صحيحة وحوالي تسعون بالمائة من أغاني بونغو فليفا تتحدث عن قضايا الحب. تمت كتابة هذه المقالة لاستكشاف موضوع الحب في مجموعة مختارة من أغاني بونغو فليفا للفنان ناسيبو عبدول، المعروف باسم دايموند بلاتينيوم.

## 1.1 Utangulizi

Nyimbo za Bongo Fleva kama zinavyofahamika ni maarufu kwa vijana kuanzia miaka 15 na kuendelea (Omari, 2009). Nyimbo hizo huwasilishwa kupitia audio na video zikihusisha mashairi, muziki na unenguaji. Nyimbo hizo ambazo pia zinafahamika kama muziki wa

*Corresponding author:
E-mail addresses: abdulfattah@yahoo.com , (M. O. Maguo) Omarymohamed36@out.ac.tz
*Article History : Received 18 February 2025 - Received in revised form 07 August 2025 - Accepted 17 August 2025*

kizazi kipya zilianza mwaka 1990 zikiwa ni zao la Hip Hope, R&B za marekani (Perulo, 2005). Hip Hope na R&B ni aina ya muziki wa kufokafoka ambao umekuwa ukiimbwa na Wamarekani wenye asili ya Afrika ikiwa kama chombo cha kuwasilisha maoni yao juu ya namna ambavyo wanataka jamii ya Kimarekani iwe. Jamii ya Kimarekani ilikuwa inaishi kibaguzi ambapo Wamarekani weusi walikuwa wakinyimwa fursa
sawa za elimu, ajira, nafasi za uongozi, huduma za afya na makazi bora. Kupitia nyimbo hizo waliweza kuelezea hisia zao juu ya ubaguzi huo na kuhitaji mabadiliko makubwa kufanyika ili kila Mmarekani awe na haki sawa na mwingine.

Kwa upande wa Nyimbo za Bongo fleva katika nchi ya Tanzania zimekuwa zikitumiwa na vijana kama chombo cha kuelezea matarajio yao na changamoto za maisha zinazowakabili ikiwa ni pamoja na uhaba wa ajira, umaskini, rushwa na ufisadi, ukosefu wa haki na maradhi hasa UKIMWI. Nyimbo za Bongo fleva zinaelezea masuala mengi kuhusu maisha katika jamii na mapenzi ndiyo yanayotajwa kuchukua nafasi kubwa zaidi (Low, 2011). Hii ni kwa sababu katika umri wa ujana mapenzi ni jambo ambalo linawasumbua vijana wengi kutokana na ukweli kuwa ni wakati wao mabadiliko ya mwili. Thompson (2008) anasema kuwa vijana wasilaumiwe kwa kuzungumzia mapenzi kwa sababu ndio wakati wao kufanya hivyo na ndio hitaji lao kubwa la maisha katika umri walionao. Maelezo haya ni sahihi na karibu asilimia 90 ya nyimbo za Bongo fleva zinazungumzia masuala ya mapenzi. Makala haya yameandikwa kuchunguza dhamira ya mapenzi katika nyimbo teule za Bongo fleva za msanii Nasibu Abdul alamaarufu Diomond Platinum.

**2.1 Mkabala wa Kinadharia**

Katika sehemu hii kumewasilishwa nadharia iliyotumika katika uandishi wa makala haya ambayo ni nadharia ya Saikolojia changanuzi ambayo ufafanuzi wake umetolewa kama ifuatavyo:

**2.1.1 Nadharia ya Saikolojia Changanuzi**

Saikolojia Changanuzi ni nadharia iliyoanzishwa na mtaalamu wa masuala ya Saikolojia anayefahamika kwa jina la Sigmund Freud katika karne ya 19. Mtaalamu huyu alifanya tafiti mbalimbali zinazohusiana na saikolojia ya binadamu na kufanikiwa kugundua masuala mbalimbali (Chapman, 2011). Anaeleza kuwa katika saikolojia ya binadamu kuna maeneo matatu ya ubongo ambayo ndiyo hufanya mwanadamu kufanya mambo mbalimbali ambayo anakuwa akiyafanya aidha kwa ufanisi au si kwa ufanisi. Maeneo hayo ni utambuzi (concious), utambuzi usio kamili (sub-concious) na kutojitambua (unconscious). Kutokana na haya ndipo kunapatikana mambo matatu ambayo ndiyo muhimu katika maisha ya mwandamu kwa kurejelea saikolojia ambayo ni mahitaji, raha na wasiwasi. Mapenzi ni dhamira ama jambo ambalo linaingia katika maeneo hayo matatu ili yaweze kustawi. Nadharia hii imetumika katika kuongoza uandishi wa makala haya yaliyolenga kuchunguza dhamira ya mapenzi katika nyimbo za msanii nasibu Abdul.

**3.1 Methodolojia ya Malaka**

Data za makala haya zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini ambayo ni mbinu ya kukusanya data kwa mtafiti kusoma matini iliyoteuliwa kwa mazingatio ili kupata data (Kothari, 2009). Data zimekusanywa kupitia hatua tano za mbinu ya usomaji makini. Hatua ya kwanza ilikuwa ni kusoma mashairi ya nyimbo za bongo fleva bila kuchukuwa madondoo ambapo mtafiti alisoma beti za mashairi husika kwa umakini ili kupata picha ya jumla kuhusu mashairi hayo, hatua ya pili ilikuwa ni kuunda mada ama vichwa kwa ajili ya kudondolea data, hatua ya tatu ilikuwa ni kusoma na kuanza kudondoa sehemu ya beti na mishororo ya mashairi ya nyimbo za bongo fleva, hatua ya nne ilikuwa kupanga data zinazofanana na kutenganisha data zinazotofautiana na hatua ya mwisho ni kupangilia data vizuri kwa namna ambayo inasaidia katika kuchambua data kwa urahisi. Baada ya kukusanya, data zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo na kushadadiwa na nadharia ya Saikolojia Changanuzi.

**4.1 Dhamira za Mapenzi**

Sehemu hii inahusu uwasilishaji wa dhamira za mapenzi kutoka katika nyimbo za msanii Nasibu Abdul.

**4.1.1 Kuteseka Kimapenzi**

Kijana katika nyimbo za msanii Nasib Abdul anasawiriwa kama mtu ambaye anasumbuliwa au kuteseka sana kimapenzi. Hii inatokana na kuwa na mpenzi ambaye anaonekana kutokuwa na mapenzi ya dhati. Wimbo wa "Moyo Wangu," unathibitisha haya hususani katika dondoo lifuatalo:

> Mmmmh tena, kutwa
> Kucha mara oohhh
> Huwezi kosa maneno, ili
> Mradi tu tara tantalila,
> Mmmh sina raha
> Wala sina tena mipango, kutwa
> Nzima na mawazo Gina
> Mmmmh aaaahh ooh sina raha ooh mama

Hapa tunamuona kijana akisawiriwa kama mtu ambaye anateseka sana na mambo ya mapenzi kutokana na mpenzi wake kuwa ni mtu mwenye maneno mengi ambayo yanamkosesha raha mwenzi wake. Hali hii inamfanya kijana kukosa muda wa kupanga mipango yake ya maendeleo na kila mara kuwa na mawazo juu ya mpenzi wake na maneno maneno kutoka kwa mpenzi huyo. Nadharia ya Saikolojia Changanuzi inatueleza kwamba, hakuna jambo ambalo linaathiri saikolojia ya mtu kama mapenzi. Hii ni kwa sababu mapenzi yana nafasi kubwa sana katika maisha ya binadamu na hivyo mtu anapokuwa na mawazo kuhusu mapenzi au mpenzi wake hakuna namna mtu huyo anaweza kuwa makini katika kufikiria mambo mengine yakiwemo ya maendeleo (Farrel, 1981). Kitu ambacho kitamfanya kijana aweze kuwa na fikra na mipango ya maendeleo ni utulivu wa nafsi ambao hata msanii Nasib Abdul anautaja katika wimbo huu huu wa "Moyo Wangu," katika dondoo hili:

> …
> Tamu ya wali ni nazi eeeeeh
> Raha ya supu maandazi eeeeh
> Raha yangu ni kupendwa
> Tu naye lakini nyota sinaa

Dondoo hili linaonyesha kuwa pale kijana anapopata mapenzi ya dhati kutoka kwa mwenzi wake anatulizana kisaikolojia na hatimaye kuweza kufanya mambo mengine ya msingi na ya maendeleo katika maisha yake. Msanii anasema, "tamu ya wali ni nazi eeeeeh na raha ya supu maandazi eeeeeh, raha yangu ni kupendwa." Maneno haya yameandikwa kwa lugha ya picha yakieleza thamani ya mapenzi na uzuri wake katika maisha ya jamii hasa kwa kijana. Kijana anapopata mapenzi ya dhati na moyo wake kuridhika anatuliza akili yake na hatimaye kufanya mambo makubwa ya kimaendeleo. Usawiri wa kijana kama mtu ambaye anakumbana na matatizo mengi katika mapenzi tunayaona katika wimbo wa "Kwa nini?" kupitia dondoo lifuatalo:

> Nikose rahaa, kisa kupendwa na we
> Nishachoshwa na haya mapenzi, visa mara mie
> kumuenzi,
> Mara hili limekwisha na
> Haya mapenzi, visa mara mie kumuenzi
> Leo limekwisha hili kesho lingine…
> Nikose raha kisa kupendwa na wewe.

Hapa tunaona kijana akilalamika juu ya mapenzi yake kuwa ni chanzo cha yeye kupata taabu na kuishi maisha ya shida. Mpenzi wa kijana huyu anaonekana kuwa ni mtu ambaye ni msumbufu na hana mapenzi ya dhati kwa mpenzi wake. Kila siku mpenzi huyo analeta jambo jipya ambalo litasababisha tafrani kwa mwenzi wake.

**4.4.2 Mapenzi ya Uongo**

Vijana wengi hivi sasa wanakabiliwa na tatizo la kukumbana na mapenzi ya uongo ambapo kijana wa kike au kiume anaweza kuwa muongo kwa mwenzake (Orange, 1995). Kijana anaweza kuwa na wapenzi zaidi ya mmoja na kila mmoja anaelezwa kuwa ndiye anayependwa. Jambo hili linatokea sana katika maisha ya siku hizi na msanii Nasib Abdul amelisawiri jambo hili katika wimbo wa "Nimpende Nani," pale anaposema:

> We nilikuwaga na mpenzi
> Akanizingua
> Hivyo nataka muenzi
> Wa haya maradhi naugua
> Isije siku muenzi naye
> Akanisumbua

Hapa tunaona mfano mzuri ambapo mhusika ambaye ni kijana akilalamika kwamba aliwahi kuwa na mpenzi lakini mpenzi huyo alikuwa na mapenzi ya uongo. Matumizi ya neno "Akanizingua," yanaashiria kuwa mwenzi huyo ni mtu ambaye alikuwa na mapenzi ya uongo kwa mwezi wake. Kama angekuwa ni mtu mwenye

mapenzi ya dhati basi asingeliweza kufanya hayo aliyoyafanya ya kumzingua mwenzake. Sasa baada ya kubaini kuwa mpenzi wake alikuwa na mapenzi ya uongo na kuachana naye sasa anatafuta mpenzi mwingine wa kuwa naye. Hata hivyo, anatoa anajipatia tahadhari kwamba:

…
Ikawa tena kitenzi
Mzigo kutwa
Naogopa sana vijana wa
Sasa kwenye mapenzi wasije
Wakanitenda nikazama na huba ya
Mapenzi ya kweli
Wakaniacha wakaenda.

Dondoo hili linamsawiri kijana kama mtu hatari sana katika mapenzi kwani wapo watu ambao unaweza kuwaamini sana katika mapenzi lakini wakafanya mambo ambayo ni ajabu ya kukuumiza moyo wako. Anasema kuwa, vijana wa siu hizi hawaaminiki katika mapenzi kwa sababu mapenzi yao ni ya uongo mtupu. Wengi wao siku hizi wanathamini sana fedha kuliko kuwa na mapenzi ya kweli na ya dhati kwa waenzi wao. Hii yote inasababishwa na tamaa kubwa ya mali ambayo vijana wa siku hizi wamekuwa nayo ambapo wanataka kupata utajiri wa harakaharaka bila kufanya kazi kwa muda mrefu. Inapotokea mpenzi wake hana uwezo wa kutosha basi anaamua kumuacha na kwenda kwa mwanaume mwingine ambaye ana uwezo mkubwa zaidi kimali ili aishi maisha mazuri zaidi. Ile dhana ya kwamba, mapenzi si fedha bali ni upendo wa ndani alionao mtu dhidi ya mwenzi wake inaonekana kupitwa na wakati siku hizi na badala yake fedha ndio kila kitu.

Msanii Nasib Abdul anaendelea kuonyesha hofu yake dhidi ya vijana katika suala zima la mapenzi na katika wimbo ule ule wa "Nimpende Nani," anasema:

Wengi ni wajanja watoto wa mjini
Wamejawa utapeli tamaa.
Wazuri ni wengi lakini kumpata
Mwenye mapenzi ya ukweli ndio balaa.

Vijana wa siku hizi wanaonekana kuwa ni watu ambao wamejawa na tamaa zaidi kuliko mapenzi na mapenzi ya kweli huonekana pale palipo na fedha. Fedha zinapokosekana tu basi kila kitu kinaharibika na kusambaratisha ndoa na familia katika jamii. Mambo haya yametokea katika sehemu mbalimbali duniani na si katika nchi ya Tanzania peke yake. Wanawake ambao wanatajwa kuwa ni wazuri wapo wengi sana lakini ambao wana maadili mazuri ni wachache sana na hawapatikani kwa urahisi siku hizi.

**4.4.3 Kubadili Wapenzi**

Kijana ni mtu ambaye anatajwa kuwa na damu ambayo inachemka na ndio wakati wake hasa kujjihusisha na masuala ya mapenzi. Katika kipindi hicho cha ujana anaweza kuwa na wapenzi wengi kwa madai ya kupimana tabia kabla ya kufikia uamuzi wa kuoana. Katika harakati hizo mambo mengi hutokea na kwa sababu hakuna binadamu ambaye ni mkamilifu basi inakuwa ni vigumu kudumu katika mapenzi yao. Pia, ni katika kipindi hiki ambapo kijana anakuwa na matamanio mengi na kila anapomuona msichana mwingine tofauti na yule wa kwake anamuona kuwa ni mzuri zaidi. Msanii Abdul ametumsawiri kijana katika hali ya kubalisha wapenzi kupitia wimbo wake wa "Sikomi," kama anavyosema:

Moyo ukaniambia Nasibu sasa Mapenzi basi
Ila nang'ang'ania najaribu kuipinga nafsi
Esma ananiambia mdogo wangu mapenzi basi
Ila nang'ang'ania
Nikiumizwa na huyu kesho nina mwingine
Ooh mbona sikomi
Sikomi
Sikomii
Licha ya mateso haya
Najiuliza (ooh sikomii)

Hapa tunaona kijana akisawiriwa kama mtu mwenye tabia ya kubadilisha wapenzi kwa sababu ya kufanyiwa mambo mabaya na mapenzi wake. Mfanya mabaya anaweza kuwa mtu yeyote kati ya watu wawili yaani mwanaume au mwanamke ambapo katika dondoo inatajwa bayana kwamba kijana wa kiume ndiye ambaye anabadilisha wanawake kila siku. Msanii Nasib Abdul anatumia nafsi ya kwanza kuonyesha kwamba yeye ni bingwa wa kubadilisha wanawake licha ya kwamba akipata matatizo na mwanamke wa kwanza haiwi fundisho kwake kuacha kutafuta wanawake wengine. Katika dondoo msanii anatumia neno "kuumizwa" akiwa na maana ya kufanyiwa jambo baya na mpenzi wake ikiwa ni pamoja na kubaini kwamba mpenzi wake ana mahusiano mengine nje na mtu mwingine. Pamoja na yote haya kufanyika lakini anasema kwamba anashindwa kabisa kuacha kufikiria mapenzi na ndio maana mara baada ya muda mfupi hujikuta tena ameingia katika mapenzi na mwanamke mwingine. Anaeleza kuwa, nafsi yake pamoja na ndugu zake wanamuonya kwamba sasa bwana mapenzi basi achana nayo lakini bado hawezi kupingana na nafsi yake. Kisaikolojia hili jambo linatajwa kuwa ni kitu ambacho kipo akilini mwa binadamu na si rahisi kwa binadamu kuiepusha na mapenzi hasa ngono ikiwa yeye ni mtu mkamilifu ambaye hana tatizo lolote lile la kibailojia (Sherwood, 2006).

Kimsingi, katika sehemu hii tumeona msanii Nasib Abdul akitumia nafsi ya kwanza kuelezea matatizo ambayo yamemkubwa katika mahusiano yake na wanawake kadhaa aliowahi kuwa nao lakini kwa upande mwingine inaonekana hata yeye mwenyewe pia kuna wakati amewahi kuingia katika mtengo wa kumuumiza mwenzi wake. Mfano dhahiri ni maneno yafuatayo:

Acha na penny we darling
Niliomuhonga gari aliponambia ana mimba
Mwisho wa siku akaichomoa chaliiii
Mola akanituniku Zari
Akanzalia dume na mwali
Nilivyo mjinga nikacheat
Aibu mpaka kwa vyombo vya habari

Dondoo hili linaonyesha namna kijana wa kiume naye anavyoweza kumuumiza mwenzi wake na kusababisha mwenzi huyo kuondoka na kuchana na mpenzi wake ambaye kimsingi bado ana mapenzi naye. Hii inatoa funzo kwamba kijana kwa hakika ni mtu ambaye ana tamaa nyingi na haridhiki hata mara moja na kile ambacho anakifanya au kufanyiwa na mwenzi wake na hivyo kuona haja ya kuwa na mpenzi mwingine nje. Hali hii imechangia katika kuwafanya vijana kuwa ni watu ambao wanatangatanga sana kimapenzi. Wasanii wengi ambao bado ni vijana wamekuwa na mahusiano na wanawake wengi kutokana na tamaa hizo ambazo wakati mwingine zinasababishwa na mazingira. Msanii anapokuwa katika matamasha yake au anapokuwa akiandaa video ya wimbo wake anaweza kukutana na msichana ambaye yeye atamuona kwamba ni mzuri sana na kuanzisha naye urafiki hatimaye kuwa mpenzi wake. Kwa sababu hakuwa amefanya utafiti wa kujiridhisha juu ya tabia ya mwenzi huyo basi mapenzi yao yanakuwa hayadumu baada ya muda wanaachana na ile dhana ya vijana kubadilisha wanawake au wenzi inaendelea kujitokeza na kujidhihirisha (Smart, 2007).

**4.4.4 Nguvu ya Mapenzi**

Kijana anasawiriwa kuwa ni mtu ambaye anayepambana sana na nguvu ya mapenzi katika maisha yake. Mapenzi ni kitu ambacho kina nguvu sana na kwamba kila anavyojitahidi kupambana na mapenzi wakati mwingine huweza hata kugombana na wazazi na ndugu zake. Haya yanathibitishwa katika wimbo wa "Kizaizai," kwamba:

Nyie mapenzi yanaumiza (Kizaizai)
Ooh kizunguzungu jamaa mapenzi mabaya
Weza gombana na ndugu (kizaizai)
Rafiki akawa mbaya (kizaizai)
Kazi ukaiona chungu (kizaizai)
Nyie mapenzi karaha (kizaizai)

Dondoo linathibitisha namna mapenzi yanavyoweza kumfanya kijana hata akawa hana tofauti na kichaa. Ikiwa kazi itakuwa chungu kwake, wazazi na marafiki wote ni wabaya atakuwa akiishi katika maisha ya namna gani? Bila shaka yatakuwa ni maisha mabaya sana ambayo yanaweza kumfanya kijana akapata matatizo ya kisaikolojia na baadhi yao kuwa vichaa kabisa. Wapo vijana wengi katika jamii ambao wamekutana na kadhia hii na yote ni ni kwa sababu ya aidha mpenzi au mwezi wake si mtu mwenye maadili anafanya mambo ya kumuumiza mwenzi wake au kijana kampenda msichana fulani na kumfanya kuwa mwenzi wake lakini wazazi au ndugu zake hawamtaki msichana huyo (Gray, 1994). Katika harakati za kutaka kupambana na wazazi au ndugu zake na kuwaonyesha kwamba yeye ndiye mwenye maamuzi na anampenda sana mpenzi wake ndipo hapo anapoumia zaidi kwa sababu ndugu nao wanajitahidi kumuonyesha kwamba huyo msichana hafai kuolewa na wewe.

Katika mazingira kama haya kijana anapata taabu sana kutokana na nguvu ya mapenzi ambayo tayari ipo moyoni mwake juu ya msichana au kijana wa kiume ambaye anampenda. Mambo haya huwakumba watu mbalimbali katika jamii na sio vijana wa kiume peke yake bali hata vijana wa kike. Kijana wa kike anaweza kumpenda mvulana au mwanaume fulani lakini wazazi wake wanamweleza kwamba sisi hatumtaki huyo kijana na hivyo hawezi kuwa mume wako. Hapo ndipo mvurugano wa nguvu ya mapenzi na nafsi ya msichana huanza kupambana. Kwa hakika nguvu ya mapenzi ni kitu kikubwa sana na kinatakiwa kitazamwe vizuri kwa kuwa kimekuwa kikisababisha matatizo ya kisaikolojia kwa vijana wengi katika jamii.

**4.5 Hitimisho**

Usawiri wa kijana na mapenzi katika nyimbo za Bongo fleva za msanii Nasibu Abdul umeonyesha kwamba kijana anasawiriwa katika maeneo ya kuteseka kimapenzi, mapenzi ya uongo, kubadili wapenzi na nguvu ya mapenzi. Kupitia vipengele hivi ni dhahiri kwamba kijana anatumia muda wake mwingi kushughulishwa na masuala ya mapenzi kuliko mambo mengine ya maendeleo katika jamii. Kutokana na matokeo haya ya utafiti wa makala haya ni kwamba vijana wanapaswa kupatiwa mafunzo na semina za ushauri nasaha mara kwa mara kuhusu masuala ya mapenzi na jinsi ya kukabiliana na changamoto zinazotokana na mahusiano ya kimapenzi. Hii itawafanya kuwa imara na madhubuti na kutofikia maamuzi mabaya ya kujidhuru pale inapotokea kuna changamoto zozote katika mahusiano yao ya kimapenzi.

**MAREJELEO**


Chapman, H.M. (2011) *Love: A Biological, Psychological and Phisiological Study*. Rode Island: University of Rode Island Press.

Farrel, B.A. (1981) *The Standing of Psycho-Analysis*. London: The Hogarth Press.

Gray, P. (1994) *The Ego and Analysis of Defense*. New York: Oxford University Press.

Kothari, C.R. (2008) *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishing Ltd.

1. Low, N.R. (2011) “Athari ya Lugha Katika Kuibua Dhamira: Mifano kutoka Nyimbo za Kizai Kipya zinazohusu UKIMWI”, Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kiukuu cha Dar es Salaam.

Omari, S. (2009) “Tanzanian Hip hop Poetry as Popular Literature”, Unpublished Ph.D Dissertation, university of Dar es Salaam.

Orange, D. (1995) *Emotional Understanding: Studies in Pschoanalytic Epistemology*. London: Guildford Press.

Perullo, A. (2005) “Hooligans and Heroes: Youth Identity and Hip Hop in Dar es Salaam Tanzania,” katika Africa Today Vol. 51 na 4 (2005): 75-101.

Sherwood, L. (2006) *Fundamentals of Physiology: A Human Perspective*. Belmont: Thomson Books.

Smart, C. (2007) *Personal Life*. Cambridge: Polity Press.

Thompson, K. D. (2008) “Keeping it Real: Reality and Representation in Maasai Hip-Hop,” *Journal of African Cultural Studies*, 20, 1 (2008): 33-44.